

Sera ya Afya na Usalama


Usalama Wangu, Usalama Wetu

Sera

Kampuni ya Tanga Cement inathamini sana watu, afya na usalama wao. Lengo letu kuu ni kutokuwa na ajali. Hivyo tunazingatia yafuatayo:

Malengo Mahususi

1. Tunaamini kuwa afya na usalama ni muhimu kwa ajili ya ushindani na upatikanaji wa faida hivyo wadau wote wanaelewa uhusiano uliopo kati ya faida, afya na usalama kazini.
2. Tumedhamilia kuzuia ajali, athari za kiafya na kuendelea kuboresha miundo na mifumo ya utendaji wetu kwa kupanga na kupitia malengo ya afya na usalama
3. Tutafikia viwango vya juu zaidi vya afya na usalama kwa kufuata hatua za kudhibiti vihatarishi, kuweka mifumo imara ya kuzuia ajali na kuanzisha utamaduni mzuri wa kuzingatia masuala ya afya na usalama.
4. Tutazingatia sheria, kanuni na taratibu nyingine za afya na usalama mahala pa kazi.
5. Tutatoa mafunzo, tutakuza na kuongeza uzoefu pamoja na ujuzi ili kuhakikisha wafanyakazi wetu wanatambua, wanaelewa, wanadhibiti vihatarishi na athari zinazohusiana na kazi zao.
6. Mitambo na vifaa vyetu vitatunzwa na kufanyiwa matengenezo kwa viwango vya juu na mabadiliko yoyote yatafanyiwa tathimini ya hatari
7. Tutawahusisha na kuwasiliana kwa uwazi na wadau wetu katika masuala ya afya na usalama.
8. Tutaripoti ajali zote, kuchambua sababu za msingi za kutokea kwake na kutafuta njia bora za kuzuia ili zisitokee tena.
9. Tutaipitia sera hii mara kwa mara ili kuhakikisha iko vizuri na inakidhi mahitaji ya wakati uliopo.
10. Sera hii itakuwa wazi kwa wadau wetu wote wa afya na usalama.

Imetolewa na,		Nambari ya Marekebisho	04
	Reinhardt Swart Mkurugenzi Mtendaji	Tarehe	Aprili 2023



SIMBA
CEMENT
STRENGTH WITHIN